

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWA
SALAMU ZA MHE. MKUU WA WILAYA YA KISARAWA KWENYE
MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU TAREHE 16.07.2018

Mhe. CHARLES FRANCIS KABEHO, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, wakimbiza Mwenge wote Kitaifa.

Wahe. Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Mhe. Katibu wa CCM Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Wahe. Viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa

Mhe. Mbunge –Jimbo la Kisarawe

Wahe. Viongozi wa Dini.

Wahe. Madiwani.

Wakuu wa Taasisi na Mashirika.

Watendaji wa Serikali, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Waandishi wa Habari. Wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya Kisarawe mliohudhuria, Mabibi na Mabwana, Itifaki imezingatiwa

MHE. KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo kwenye mapokezi ya Mwenge wetu wa Uhuru

Nawapongeza sana wakimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa kuukimbiza Mwenge wetu wa Uhuru salama na kueneza ujumbe wa Mwenge kwa Wananchi wenzetu.

MHE. KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA

Katika Halmashauri za Wilaya ya Kisarawe, Mwenge wetu utakimbizwa kwenye umbali wa Km. 294.3 katika Tarafa 4 za Sungwi, Maneromango, Chole na Mzenga, Kata 7 na vijiji 9. Aidha Mwenge wetu wa Uhuru, utaweka Jiwe la Msingi kwenye mradi mmoja (1), kuona na kukagua miradi minne (4), kuzindua miradi miwili (2). Pia katika eneo la mkesho, Mwenge wa Uhuru utatembelea mabanda ya UKIMWI, Malaria, Madawa ya Kulevya na Rushwa

MHE. KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mwenge wa Uhuru Miradi yote hii imegharimu jumla ya Tshs.6,234,109,545.00 kwa mchanganuo ufuatao; Wananchi 8,844,000.00 Halmashauri 32,560,000.00, Serikali Kuu 6,192,705,545.00

MHE. KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe wapo tayari kupokea na kuufanyia kazi ujumbe wa Mwenge wa Uhuru mwaka huu 2018 usemao **UWEKEZAJI KATIKA ELIMU CHINI YA KAULI MBIU “ELIMU NI UFUNGUO WA MAISHA WEKEZA SASA KWA MAENDELEO YA TAIFA LETU”** Lengo la ujumbe huu ni kuelimisha, kuhimiza, kuisitiza na kufafanua kwa wananchi umuhimu wa kuwekeza katika elimu kwa kuboresha miundo mbinu, kuhimiza masomo ya sayansi na dhana ya mpango wa serikari wa elimu bila malipo. Aidha Mwenge wa Uhuru unaendelea kuhamasisha wananchi juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria, Rushwa pamoja na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Aidha tunaendelea kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika maeneo yao bila kujali Dini, Kabila, Rangi au mlengo wa chama cha siasa ili kuendana na dhana ya ushirikishwaji

MHE. KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA

Wananchi wa Halmashauri za Wilaya ya Kisarawe wana hamu kubwa sana kuuona Mwenge wa Uhuru na kuusikia ujumbe wa Mwenge, hivyo niwashukuru wote kwa kunisikiliza na nitamke sasa kwa heshima na taadhima kwamba tuko tayari kuanza Mbio za Mwenge wa Uhuru wa 2018. Nitahakikisha usalama wa Mwenge wa Uhuru na msafara wote kwa jumla.

Naomba kuwasilisha

MWENGE OYEEEEEEEEEEEEEE!!

.....

Happiness Seneda

MKUU WA WILAYA

KISARawe